

## UPANZI


- Chimba mashimo ya upanzi kwa nafasi ya futi 3 (cm 90) kati ya mistari na futi 2 (cm 60) kati ya mimea.
- Katika kila shimo:-
  - Tumia mbolea ya shamba mkono mmoja
  - Tia fatalaiza ya DAP kifuniko kimoja cha soda



SHIMO TAYARI KWA UPANZI



TIA MBOLEA YA SHAMBA SHIMONI



TIA FATALAIZA YA DAP SHIMONI

MBEGU ZA KUPANDA




MUWA YA NAPIA




SHINA LENYE MIZIZI

- Weka muwa yenye vifundo vitatu ndani ya shimo na uhakikishe vifundo viwili vimefukiwa ndani ya udongo au
- Fukia shina lenye mizizi ndani ya shimo.




WEKA MUWA NDANI YA SHIMO



MUWA UMEFUNIKWA NA UDONGO BAADA YA UPANZI

- Palilia shamba kuondoa makwekwe yote.




### Napia inavunwa lini na namna gani?

- Vuna napia ikitimia miezi 2-3 au ikifika urefu wa futi 3-4.
- Anza kuvuna msitari ya kando kando kuzunguka shamba lote. Uwape majani haya kwa mifugo wako.
- Kisha vuna mistari ya ndani ukiacha muda kwa mistari ya kando kando kumea tena.

### Kwa nini ni vizuri kukuza napia kuzunguka mahindi yako?

Utapata mahindi, chakula, maziwa zaidi, pesa nyingi na utalinda udongo yako

Utapata:

- **Mahindi zaidi kwa sababu uharibifu wa mabuu umepungua.**
- **Majani mabichi kwa mifugo wako mwaka mzima.**
- **Ikiwa huna mifugo basi unaweza kuyauza majani.**
- **Napia inakinga mahindi kutokana na upepo mkali. Mimea haitaangushwa na upepo.**
- **Udongo una unyevu na haukauki haraka.**
- **Napia inashikanisha udongo pamoja na inazuia maji yanayotiririka na mmomonyoko wa udongo.**

Imetayarishwa na Mediae Trust
PO Box 39486 Nairobi. Tel 442660

# Kuza Mahindi na Napia Zaidi Upate Pesa Nyingi



**Zuia buu la mahindi kwa kupanda napia kuzunguka shamba lako la mahindi. Napia itawanasa wadudu hawa.**

Wadhamini:
Gatsby Charitable Foundation,
ICIPE, IACR- Rothamsted,
KARI na Wizara ya Kilimo, Kenya

## Je, umewahi kuona uharibifu wa mahindi wako unaosababishwa na mabuu wa mahindi?

Inaonekana hivi. Buu -

anakula majani ya mahindi



anatoboa shina la mahindi na anakula sehemu za ndani



Iwapo ungevuna magunia 10 ya mahindi, buu atasababisha upotevu wa magunia matatu.




## Buu anaingiaje ndani ya mahindi yetu?

Ni sharti tujue mzunguko wa maisha ya buu




## Napia inazuia buu namna gani?

- Nondo wanapenda kutaga mayai juu ya napia kuliko kutaga juu ya mahindi.
- Nondo 7 kati ya 10 watataga mayai juu ya napia lakini nondo watatu watataga mayai juu ya mahindi.



- Funza akitoboa shina la napia gundi inayonata inachururika na hii inanasa funza na hatimaye anakufa.




Kwa hivyo, mafunza wachache wanaishi na mahindi yanaokolewa.

## Unapandaje napia kwa ajili ya kuzuia mabuu?

- Panda napia (aina ya Bana ni bora zaidi) kuzunguka shamba lako la mahindi.
- Katika mwaka wa kwanza panda napia kabla ya mvua ili napia iwe mrefu kuliko mahindi. Nondo watapendelea napia mrefu kuliko mahindi.
- Panda mistari mitatu ya napia kuzunguka shamba la mahindi.

